



JIANDAE KWA MAJIRA YA THELUJI







Kwa kawaida, majira ya theluji mjini Buffalo ni kuanzia mwezi wa kumi na moja mwakani hadi mwezi wa tatu wa mwaka ujawo

Theluji inaweza kuwa inchi chache hadi futi kadhaa

Tusipopata dhoruba kubwa, maisha, mashule pamoja na kazi vinaendelea kama kawaida. Hata tukipata dhoruba kubwa, mji wa Buffalo unaondoa theluji barabarani bada ya siku moja au mbili

Baada ya kupata maelezo ya kuwa theluji inakaribia eneo ya mji, tafadhali jitayarisha



- Uwe na chakula kinachoweza kudumu siku tatu nyumbani 
- Uwe na madawa ya maagizo ya mganga ya kutosha nyumbani 
- Uwe na chakula cha watoto cha kutosha, pamoja na madaipa ya kuvalisha watoto 
- Jaza chaji ya simu yako ya mikononi; ukiweza, kaa na chaji ya badala 
- Kaa na tochi na mishumaa, iwapo umeme utakatika 
- Juwa kwamba watoto wanaweza kulazimishwa kubakia nyumbani, wakati kazi inaendelea kama kawaida 
- Ondoa theluji katika njia ya kuelekea mlangoni kwako, pamoja na fasi mbele ya nyumba yako, ili baruwa za posta ziweze kuwekwa kwa sanduku lako la posta.

